



Mkutano Mkuu wa Ishirini na Saba wa Wanahisa

Mwenyekiti na Wanahisa,

Yah: Taarifa ya Mkutano Mkuu wa Ishirini na Saba

Taarifa inatolewa kwamba **Mkutano Mkuu wa Ishirini na Saba** wa CRDB Bank Plc utafanyika siku ya Jumamosi tarehe **21 Mei 2022**, katika **Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC)**, Ukumbi wa Simba na kwa njia ya kidijitali kuanzia saa tatu kamili (**Saa 3.00**) asubuhi kujadili dondoo zifuatazo:

1. Kufungua Mkutano.
2. Kuridhia Dondoo.
3. Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Ishirini na Sita.
4. Kujadili yatokanayo na kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Ishirini na Sita.
5. Kujadili na kupokea Ripoti ya Wakurugenzi wenye dhamana ya Uongozi na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za mwaka 2021.
 - 5.1 Ripoti ya Wakurugenzi wenye dhamana ya Uongozi.
 - 5.2 Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2021.
 - 5.3 Gawio kwa mwaka 2021.
6. Kuidhinisha ada ya Wakurugenzi.
7. Kuteua Wakaguzi wa Hesabu.
8. Kuchagua Wajumbe wa Bodi
 - 8.1 Wajumbe watatu (3) wa Bodi watakaowakilisha kundi la wanahisa wenye hisa chini ya asilimia moja (1%).
 - 8.2 Mjumbe mmoja (1) wa Bodi atakayewakilisha kundi la wanahisa wenye hisa kati ya asilimia moja na kumi (1% na 10%).
 - 8.3 Mjumbe mmoja (1) Huru wa Bodi
9. Kujadili mapendekezo kutoka kwa Wanahisa.
10. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.
11. Kupanga mahali na tarehe ya Mkutano ujao.
12. Kufunga Mkutano.

MAELEZO

1. **Mahudhurio kwa njia ya Kidijitali:** *Mwanahisa anaweza kuhudhuria Mkutano Mkuu kwa njia mbalimbali za kidijitali (SIM Banking, SIM Account na tovuti [<https://www.crdbbank.co.tz>]). Benki itawatumia wanahisa wote kupitia simu zao za mkononi utambulisho na maelekezo kuhusu jinsi ya kujiunga na kushiriki Mkutano Mkuu kidijitali.*
2. **Daftari la Wanahisa litafungwa** tarehe 13/05/2022 na litafunguliwa tena tarehe 16/05/2022.
3. **Mapendekezo kutoka kwa wanahisa yatakayojadiliwa katika dondoo namba 9 yatumwe na yamfikie Katibu kabla ya Ijumaa tarehe 06/05/2022 saa 10.00 jioni.**
4. **Makabrasha ya Mkutano Mkuu yatapatikana matawini na yanaweza kuchukuliwa kuanzia tarehe 10/05/2022, yatapatikana pia Arusha kwenye ukumbi wa Mkutano tarehe 20 hadi 21 Mei 2022.** Pia makabrasha ya Mkutano Mkuu yatapatikana kwenye tovuti ya benki kuanzia tarehe 10/05/2022.
5. **Wanahisa wanaotaka kuhudhuria Mkutano Mkuu watajigharamia usafiri na malazi.**

TAARIFA YA SEMINA KWA WANAHISA

Taarifa inatolewa kwamba kutakuwa na Semina kwa Wanahisa itakayolenga kutoa elimu kuhusu Umuhimu na taratibu za kuandaa Wosia na Mirathi, Kusitisha utoaji wa Risiti za Uwekezaji na Umuhimu wa kulinda Mali zako itafanyika Ijumaa, tarehe 20/05/2022 katika **Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC)**, Ukumbi wa Simba kuanzia saa **3.00** asubuhi.

Kwa mawasiliano tumia anuani ifuatavyo:

Katibu

CRDB Bank Plc

CRDB Bank Head Quaters

S. L. P. 268

Dar-es-Salaam

Simu. na. 022 - 2114237, 2117442 - 7 - Fax na. 022 - 2131005

Barua pepe -shares_unit@crdbbank.co.tz

KWA IDHINI YA BODI

J. B. Rugambo

KATIBU

20 Aprili, 2022